



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU UAMUZI WA RUFAA DHIDI YA UAMUZI WA MSIMAMIZI
MSAIDIZI WA UCHAGUZI WA KUTOWATEUA WAGOMBEA WA
UDIWANI KATIKA KATA YA BWONGERA, HALMASHAURI YA
WILAYA YA CHATO, MKOA WA GEITA

Dodoma, Tarehe 15 Mei, 2026

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 65(7) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sura ya 343, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imepokea rufaa tano (05) za wagombea Udiwani wanaopinga uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wa Kata ya Bwongera wa kutowateua kuwa wagombea.


Katika kikao chake maalum kilichofanyika leo tarehe 15 Mei, 2026, Tume imesikiliza rufaa mbili (02) kati ya rufaa tano (05) zilizowasilishwa na kuzikubali kama ifuatavyo: -

- i. **Ndugu Anastazia Peter Bampiga** mgombea Udiwani kupitia Chama cha UPDP dhidi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Kata ya Bwongera; na
- ii. **Ndugu Ramlath Ramadhan Abdul** mgombea Udiwani kupitia Chama cha N.L.D dhidi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Kata ya Bwongera.

Hivyo, wagombea tajwa, wamerejeshwa katika orodha ya wagombea Udiwani katika kata husika na waendeleo na taratibu za kampeni za uchaguzi mdogo wa Udiwani utakaofanyika tarehe 01 Juni, 2026.

Aidha, rufaa tatu (03) zilizobaki zitasikilizwa na kutolewa uamuzi katika kikao cha Tume kitakachofanyika Jumatatu tarehe 18 Mei, 2026.

Imetolewa na:


Kailima, R. K

MKURUGENZI WA UCHAGUZI

